
# KUSADIKIKA



Shaaban Bin Robert


KUSADIKIKA
Shaaban Bin Robert

# KUSADIKIKA

## Nchi iliyo kwa anga

Shaaban bin Robert

# YALIYOMO

Mashtaka

Uanasheria

Mjumbe wa Kaskazini

Mjumbe wa Mashariki

Mjumbe wa Kusini

Mjumbe wa Magharibi

Mjumbe wa Mbinguni

Mjumbe wa Ardhi

Hukumu

Ngombe avunjikapo guu lishoni hujiburuzia zizini kujisitiri

# MASHTAKA

Waziri wa kusadikika alikuwa mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi. Kwa hivi aliitwa Majivuno. Uwaziri wake ulianza zamani sana. Alikuwa waziri wa wafalme watatu katika nyakati mbalimbali. Babu yake mfalme anayesimuliwa aliposhika ufalme, yeye alishika uwaziri; baba yake alipokuwa nahodha wa chombo cha serikali, yeye alikuwa rubani wake; akaendelea katika hadhi hiyo mpaka wakati wa enzi ya mfalme mpya. Umri wake mkubwa ulizifanya nywele zake kichwani kuwa nyeupe,

Kwa haiba hii aliweza kuyavuta macho ya watu; na kwa ufasaha wa maneno aliweza kufanyiza fungu au mwamba wa kuyavunja maisha ya mtu yeyote kama chombo. Kipawa chochote cha mtu kama hakikuongozwa vema huweza kuwa hatari au maangamizi kwa wengine. Mtu huyu alikuwa maarufu na mashuhuri lakini alijaa tadi na inda kama hadithi hii inavyosimulia.

Majivuno aliyaanza mashtaka yake kwa kusema hivi, “Jalali mfalme na madiwani wakuu wa baraza. Nataka kuweka mbele yenu mashtaka ya serikali ya Kusadikika juu ya Karama, raia mmoja, anayelindwa na ulinzi wa mfalme, lakini si mwaminifu; anayefaidi haki na mapendeleo ya utawala huu, lakini hana shukrani; na aliye chini ya bendera ya nchi hii, lakini si mtii. Miaka kumi imepita tangu mnong’ono wa kwanza ulipofika katika sikio langu kuwa mshtakiwa alikuwa mtu mwenye bughudha nyingi juu ya taratibu za utawala wa Kusadikika, na hasa juu ya hukumu zilizotolewa na mahakimu katika baraza. Ilisemwa kuwa mshtakiwa alidai kuwa hukumu chache sana zilikuwa za haki, lakini nyingi zilikuwa za dhuluma tupu. Kwanza mimi sikufikiri kamwe kuwa hili liliweza kutoka katika kinywa chake, na hata kama lingewezekana niliona ni tone moja la maji haliwezi kuleta gharika katika nchi.”

“Baadaye mnong’ono uleule wa kwanza ulikaririwa katika sikio langu. Lakini sasa niliambiwa kuwa mshtakiwa alikuwa kiongozi mwenye wafuasi wengi waliokuwa wakijifunza uanasheria chini yake. Ukariri huu ulinishtua sana. Niliona kama radi imenipasukia ghafla bila ya kufanya wingu ingawa

nilikumbuka waziwazi kuwa habari za mshtakiwa nilikwisha zisikia zamani. Tone dogo la maji, lile nililodhania kuwa litakauka lenyewe mara moja, limekuwa mlizamu wa kuwafariji kwa siri wanafunzi wa mshtakiwa! Palepale niliagiza upelelezi kuwa nyuma ya nyayo za mshtakiwa. Upelelezi huo ulidhihirisha bila ya shaka yoyote kuwa mshtakiwa alikuwa akiwafunza watu, siyo kuomba msamaha na huruma katika baraza tu, lakini hata kuzibatilisha hukumu za baraza za kusadikika kwa njia zote. Hili lilionyesha kuwa mgogoro mkubwa sana utakuwako kati ya sheria za nchi na watu wake"

"Ilipoonekana kuwa matendo ya mshtakiwa yalikuwa hayavumiliki, na yenye hatari kubwa kabisa katika nchi, niliamuru akamatwe na kuhukumiwa. Alipofika mbele yangu mara ya kwanza aliulizwa kama alikuwa mwalimu wa wanasheria. Alikubali upesi kama aliyeona ametunukiwa hadhi kubwa. Wa aidha alisema kuwa nafasi ya mwanasheria katika nchi ilikuwa tupu. Kwa hivi alikusudia kuwa mwanasheria wa kwanza wa Kusadikika.

Nilimwambia kuwa wakati ulikuwa umewadia wa kukoma kujidanganya yeye mwenyewe na watu wengine tena kwa matumaini ya kuwa mwana hivi au mwana vile bila idhini ya serikali. Nataka ifahamike waziwazi kuwa mimi nina hofu kubwa sana juu ya mshtakiwa. Sababu za hofu yangu ni kuwa, kama ikiamriwa kuwa kama atakavyo leo, kesho atadai udiwani, kesho kutwa uwaziri, na baadaye ufalme. Kwa desturi, tamaa za watu kama yeye zitaamka. Tamaa hizo zikiamka hazitakuwa na mpaka. Watu kama hao lazima wafunzwe kuzijua hali zao zilivyo katika maisha, na mwisho wa tamaa zao vilevile."

"Matendo ya mshtakiwa yalipasa kukomeshwa yalipoanza. Walakini kwa sababu ya tabia yangu njema, na saburi ambayo kila waziri lazima kuwa nayo, mashtaka haya sikuyaleta barazani mpaka leo. Nilidhani kuwa mshtakiwa akiona kuwa bidii yake ilikuwa kazi ya bure, atakoma mwenyewe kuyadhihaki mamlaka ya serikali. Badala ya kukoma, alijiona amepata nafasi ya kuyaeneza bila ruhusa ya serikali mafunzo yake yasiyotakiwa katika nchi ya kusadikika."

"Jalali mfalme na madiwani wakuu, mtakumbuka kuwa tangu zamani matendo makubwa yoyote yaliamriwa kuanzishwa na kutendwa na watu

wenye nasaba bora kama wafalme na madiwani. Watu wa ovyo kama alivyo mshtakiwa hawakuachiwa kujishughulisha na mambo yaliyo zaidi ya yale yaliyohusiana na maisha yao wenyewe tu. Kama wangaliamriwa kujishughulisha na mambo yaliyowapita vimo vyao, kama mshtakiwa aonekanavyo kuwa ndilo kusudi lake, mabadiliko ya kuchukiza yangalikuwako mara kwa mara katika nchi hii.

"Mikono ya mshtakiwa ni mifupi kwa kutenda wema wowote. Kwa hali kama hii nachelea kuwa akiamriwa kuinyoosha katika matendo makubwa matokeo yake yatakuwa mchafuko, uasi na maangamizi. Jumla ya watu kama yeye alivyo itazidi. Watu kama hao hawatakuwa raia wema ila mabarakala. Mchwa ukikaribia kuangamizwa hufanywa kumbikumbi na huoteshwa mabawa mawili. Matendo ya mshtakiwa yamekwisha kuwa mabawa ya kutosha kuifanya serikali kufikiri kama yasingepasa kukomeshwa kabisa kwa mfano uwezao kumzuia mtu mwingine yeyote kuyaigiza."

"Wafalme na raia wa kusadikika tangu zamani walikuwa, na hata sasa, ni watu wasiosema uongo. Mzee kwa kijana, mwanaume kwa mwanamke: mkubwa kwa mdogo, mvulana kwa msichana-wote wanaaminika: katika maandiko ya maamuzi ya Kusadikika hapana mwanamume fulani alisema uongo kwa kusudi la kulificha kosa. Haipatikani habari yoyote katika mapokeo ya nchi hii isimuliayo kuwa mwanamke fulani alisingiziwa hatia. Kwa imani kama hii Kusadikika imefanya maamuzi ya haki siku zote, na imetukuka ulimwenguni kama nyota ya mwongozo wa haki."

"Imani ya Kusadikika ni nguzo imara ya majengo ya utawala wa Kusadikika. Wakati mataifa mengine yalipojifaharisha kwa mambo kama vile enzi, uwezo na fahari nyingine, taifa la Kusadikika lilijivunia kwa sababu ya kusadiki mambo yaliyotoka vinywani mwa watu wake. Wasadikika walikuwa, wamekuwa, na hata sasa, ni watu wanaoijali sana imani hii kama wayajalivyo maisha yao na vitu vingine vipenzi. Haidhaniwi kuwa ruhusa ikitolewa ya utaalamu mwingine zaidi ya kusadiki kwa vijana wa nchi hii italeta faida yoyote kwao. Shaka kubwa inatuhumiwa kuwa utaalamu mwingine ukiamriwa hapa, matata yaliyokuwa bado kuonekana na wazee wetu, sisi wenyewe, wala kusimuliwa katika hadithi za

Kusadikika yatatokea kwa wingi. Tokeo la mashaka hayo, licha ya serikali ya Kusadikika peke yake, lakini hata raia hawalitaki.”

“Nilizungumza shauri hili kwa uangalifu mwingi na watu walio maarufu na walioipatia sifa Kusadikika: bwana Taadabuni , katibu wa serikali, bwana Komeni, amiri jeshi, bwana Fujo, mlinda hazina, bwana Boramimi, Mudir wa sheria, na wateule wengine. Ilionekana kuwa kuamuru taaluma ya uanasheria katika Kusadikika ni sawasawa na kuyapa nafasi mabishano katika nchi. Kwa hivi, hapana mtu hata mmoja aliyeliafiki shauri la kuyaamuru mafunzo haya. Nafasi kama hiyo ikipata idhini ya serikali, yahofiwa kuwa hatari kubwa itazikabili siasa za utawala wa nchi. Dhuluma itakuwa na kiti katika baraza za hukumu kushindana na haki. Jinai itatoka katika uficho wake ili irande uwanjani kuvutana na adili. Uhalifu utawatukuza waasi na wavunja sheria; na dharau itafunua kinywa chake kutema mate ya sumu kama bafe juu ya mamlaka ya serikali. Kwa mambo hayo, imani ya nchi pamoja na misingi yake, itakuwa katika maangamizi yadhaniwayo kuwa kitu chochote kikitumbukia ndani yake hakiwezi kuokoka tena.”

“Kwa sababu ya kudumisha sheria, dini na mamlaka; na kwa wajibu wa kazi yangu, lazima nidhihirishe mbele ya baraza hii kuwa si jambo jema hata kidogo kuamuru madarasa ya utaalamu na uwezo kuwa daraja, ambalo chini yake utapita mkondo mkubwa sana wa mambo ya kuichafua salama ya Kusadikika kwa dharau, ukaidi na jinai. Matendo ya mshtakiwa lazima yakomeshwe kwa adhabu ya mwisho katika sheria. Kazi kubwa na yenye thamani adhimu ilitendwa katika kuzitengeneza na kuzidumisha sheria hizi. Haivumiliki kuziona zinavunjika kwa matendo ya mtu mmoja anayetafuta ubarakala, asiyeaminika, mchache wa shukrani na mjeuri. Nguvu ya sheria ya nchi lazima ithibitishwe juu yake ili mtu mwingine yeyote asithubutu kuzidharau.”

# UANASHERIA

Baada ya usemi wa waziri, baadhi ya watu wachache walimsikitikia mshtakiwa, lakini wengi walikuwa wakinong'onezana kuwa msiba wa kujitakia hauna kilio. Kama watu waliokusudiwa kuwa mwenge kwa wengine wangalikuwa wakingojea shangwe la watu kabla ya kuanzisha makusudi yao, maendeleo yangaliadimika. Kwa bahati njema, mtu yeyote katika hawa hutegemea mwongozo usiotaka shangwe mpaka umefaulu. Basi itaonekana halafu kama mshtakiwa alikuwa akiyahatarisha maisha yake bure au heri ya wasadikika wote, na kwa fahari ya sheria za nchi yao.

Sheria za wasadikika zilikuwa hazimwamuru mshtakiwa kujitetea juu ya ushahidi wa mshtaki. Aghalabu mashtaka mengi yalikubaliwa bila swali wala kiapo. Labda hii ndiyo sababu ya nchi yao kuitwa kusadikika. Kama mashtaka yaliletwa mbele ya baraza za wafalme, watoto wao, matajiri, au watu wengine maarufu nguvu ya desturi hii ilifanywa maradufu. Hapana shaka kuwa salama ya watu wadogo ilikuwa kidogo sana katika nchi hii. Lakini mashtaka juu ya uanasheria yalikuwa ni habari ngeni kabis

a. Wasadikika walikuwa bado kusikia utaalamu huu. Kwa hamu kubwa ya kutaka kujua maana yake baraza lilitamani mshtakiwa kuamriwa kueleza maana ya uanasheria kabla ya hukumu kufanywa.

"Majivuno, mtu anayejinasibu mwenyewe kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa na miili ya wasadikika wote ikiwekwa pamoja, alikuwa amejifunga kwa kumtosa mshtakiwa katika bahari ya maangamizi. Kwa hivi, alisema kwa werevu kuwa uanasheria ungewezekana kutafsiriwa waziwazi sana na Mudir wa sheria za Kusadikika kuliko mshtakiwa. Mudir wa sheria alipotakiwa kufanya tafsiri alisema, "uanasheria ni elimu ya kupingana na sheria."

Kabla ya mkono ulionyooshwa na waziri haujapokewa na Mudir wa sheria, baadhi ya watu wa baraza walionyesha kuwa hawakutosheka na tafsiri hii. Walifikiri kuwa hapana mtu mmoja kati ya watu mia aliyeweza kuyapoteza maisha yake bure kwa sababu ya kupingana na sheria.

Mshtakiwa alikuwa si mjinga wa adhabu zilizohusu kutolewa kwa sababu ya hatia au uhalifu wowote.

Ilionekana kuwa maana hasa ya uanasheria ilikuwa bado kutolewa. Wazo hili lilipotolewa, mfalme alishawishika kuwaza kuwa kitanda usichokilalia huwajui kunguni wake, na kuwa ilikuwako sababu njema ya kumwamuru mshtakiwa kueleza mwenyewe maana ya uanasheria na sababu zake.

Hili lilipotokea mshtakiwa alipata nafasi ya kujitetea. Nafasi hii hakuitazamia kuipata kwa rahisi. Jinsi ilivyotokea ilikuwa kama ajabu tupu. Alishukuru kuwa uko mkono wa uokovu unaofanya kazi kwa siri siku zote. Kwa wasifu wa nje, mshtakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu, lakini kwa wasifu wa ndani, alikuwa na ajabu tatu. Kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima, kifuani alikuwa na moyo wa ushujaa, na kinywani ulimi wa ufasaha. Vipawa hivi vilikuwa katika siri kubwa sana. Hata baadhi ya wasiri wake hawakuweza kukisia kuwa alikuwa na hazina kama hizi. Alikuwa na tabia ya kuficha siri kama kaburi lifunikavyo maiti. Alijizoeza kutumia vipawa hivi mpaka vilikuwa tayari kutumika siku yoyote katika maisha yake.

Siku muhimu iliyoandaliwa matumizi ya vitu hivi ilikuwa imewadia. Maisha yake mwenyewe yalikuwa katika hatari kubwa. Pigano la kufa na kupona lilikuwa mbele yake. Alikuwa hana silaha nyingine za kuokolea maisha yake ila zana hizi. Wajibu wa kuzitumia kwa dhahiri ulikuwa hauzuiliki sasa. Basi pale kizimbani alipokuwa amesimama wima aliinama kwa unyenyekevu mbele ya baraza. Alipoinuka, kwa sauti ya taratibu lakini imara, aliyavuta masikio ya baraza nzima kumsikiliza kama imamu aliyekuwa akihutubu juu ya mimbari ya msikiti mkubwa.

Aliyosema ndiyo haya:

” Msema kweli hukimbiwa na marafiki zake. Nikipatwa na ajali kama hiyo sitaona wivu juu ya watu wawezao kudumu na marafiki zao siku zote. Siwezi kuikana kweli kwa kuchelea upweke wa kitambo, nikajinyima ushirika wa milele unaotazamiwa kutokea baada ya kushindwa kwa uongo. Yaonekana kama Mudir wa sheria mheshimiwa hakufikiri sana alipotafsiri kuwa uanasheria ilikuwa ni elimu ya kupingana na sheria.”

“Uanasheria ni elimu ya hukumu kwa mujibu wa sheria zilizokubaliwa. Hakuna kitu chochote katika utaalamu huu cha kuhofia kuwa pingamizi katika sheria. Elimu hii hasa husaidia sheria kuenda katika njia ya haki. Haina budi kukumbukwa kuwa kugawanya haki kwa watu ni dhima itakayo hekima, hadhari na saburi yote iwezekanayo kufanywa na mwanadamu.”

“Nimeshtakiwa kuwa nikiridhiwa haja nitakayo leo, halafu nitadai kuwa diwani, waziri au mfalme. Tuhuma kama hii haina msingi, utawala na mamlaka yake ni dhima ya mwanadamu. Mashetani, majini na malaika hawana kazi kama hizi. Kwa kuwa mimi ni mwanadamu, na midhali kazi hizi zimeshikwa na wenzangu, wajibu wangu ni kuchagua kazi nyingine.

“Ilinitokea kuwa Kusadikika ilikuwa na haja ya elimu ya uanasheria. Nachelea kuwa sababu zilizoniongoza kufikiria kama nilivyofanya, zitataka muda wa siku sita kuzieleza kwa muhtasari. Kama kwa muda sitaonekana kuwa nimechelewa kuitikia wito wa hukumu inayokusudiwa kutimizwa juu yangu kwa mashtaka yaliyoletwa hapa, nitakuwa tayari kuzieleza”

Waziri alitaka shauri la mshtakiwa likatwe siku ileile. Hila za kufanyizia hivyo alikuwa nazo. Kwa hila zake nyingi kama jozi ya karata alisema, “mshtakiwa ana maneno mengi kama kitabu. Nakanusha kuwa ajua kitu chochote kuhusu hekima. Hekima ni kitu adimu kupatikana na mtu asiye na mvi. Weusi wa nywele za mshtakiwa waonyesha waziwazi ujinga alionao. Nataka athibitishe kuwa nisemayo si kweli.”

Mshtakiwa alijibu, “elimu ilipokuwa haijulikani duniani, mvi zilihesabika kuwa alama ya hekima. Fikira hii ilikuwa njema sana, lakini wakati wake umepita wala hairudi tena. Sasa kama mtu hakuelimishwa, mvi zake hazihesabiwi kuwa dalili ya hekima. Jambo lisilobadilika ni kuwa kila mzee anastahili heshima ya kila kijana siku zote.”

Mfalme hakuona sababu ya haraka ya kulikata shauri la mshtakiwa. Kwa hivi, alisema kuwa mshtakiwa alitaka muda wa siku sita ili atimize kazi iliyotakiwa na baraza hili. Hakutaka kutolewa katika gereza. Yumo katika gereza na atakuwa katika hali hiyo hadi mwisho wa maelezo yake. Maelezo yatakayopatikana kwake yatakuwa faida ya baraza. Muda huu ukiisha, hukumu inayostahili itatolewa kwa mshtakiwa. Wakati una mabawa kama ndege. Uvumilivu ukitumiwa siku sita ni sawasawa na saa sita. Kwa kuwa

haifai kuonekana baraza haina saburi, haja ya mshtakiwa ya muda wa kueleza sababu za kuanzisha uanasheria katika nchi hii haina budi kukubaliwa. Hili liliposemwa, baraza liliahirishwa.

Hii ilikuwa siku ya kwanza ya muda ulioamriwa. Baraza lilihudhuriwa na mfalme, waziri pamoja na viongozi wengine wa serikali. Sudusi moja ya watu wa Sadiki, mji mkuu wa Kusadikika, walikuwepo vilevile. Mbele ya baraza hii, Karama, mshitakiwa alisimama kujitetea bila kutetemeka. Alisema kwa makini kama mtu aliyezoea kusema hadharani.

# MJUMBE WA KASKAZINI

"Ninazo sababu sita za kusema. Sababu ya kwanza iliyotia azima katika moyo wangu ya kuanzisha uanasheria katika nchi hii labda itaelezeka vema sana kama nikitaja mkasa wa mjumbe wa kaskazini uliotokea hapo zamani kidogo. Itakumbukwa kuwa mkasa huu ulikuwa mkubwa katika mikasa adhimu iliyopata kushuhudiwa na Kusadikika."

"Ilifikiriwa hapa kwamba lilikuwa jambo jema nchi hii kupeleka wajumbe katika nchi ngeni. Kusudi la ujumbe huo lilikuwa kutalii mambo katika nchi hizo yaliyowezekana kuletwa hapa kwa manufaa ya nchi na watu wake. Ilikubaliwa kuziomba nchi zilizopakana na Kusadikika kama ziliweza kuamuru wajumbe wetu kuzizuru nchi zao.

Kusadikika ilikuwa tayari pia kupokea wajumbe wa nchi nyingine kama haja yetu ilikubaliwa na nchi hizo."

"Upande uliochaguliwa kwanza kwa ujumbe huu ulikuwa kaskazini. Urefu wa safari hii haukuwezekana kupimwa; na dhiki zake zilikuwa ngumu kukisiwa kwa usahihi wowote. Hii ilikuwa ni safari ya ujasiri iliyotaka uthabiti na moyo wa matumaini. Mtu mwenye heshima, hodari na mwaminifu alitakiwa ajitolee mwenyewe kwa safari hii."

"Tumaini la kupatikana mtu mwenye heshima, uhodari na uaminifu lilikuwa dogo sana. Kwa desturi, maisha huwaficha watu wake bora mpaka tokeo kubwa litokee. Tamaa ya kumpata mtu aliyetakiwa ilipokuwa karibu kukatika, Buruhani alijitolea mwenyewe. Buruhani alikuwa mtu mwenye sifa zilizotakiwa na zaidi. Alitokea wakati nchi yake ilipomtaka sana akajitwisha mzigo mzito sana. Kazi yake ilikuwa kusafiri, kutalii na kuandika habari za mambo ya nchi ngeni aliyofikiri kwamba yaliweza kuistawisha Kusadikika."

"Ujumbe huu ulikuwa na dhima kubwa. Kama zamani wasafiri walivyoondoka katika nchi walizozijua na kusafiri katika nchi walizokuwa hawazijui, msafiri huyu pia alikujua alikotoka lakini hakukujua alikokwenda. Hakujua kama mbele alikuwa akingojewa na msaada wa

kumsaidia au maangamizi ya kumwangamiza. Alijitolea sadaka katika ujasiri ambao misiba yake ilikuwa katika mwangaza, lakini faraja zake zilikuwa katika kiza kikuu."

"Alisafiri kuelekea kaskazini kwa moyo wa kufanikiwa safarini, na kwa matumaini ya kurudi kwao salama. Safari yake ilimpitisha katika misitu mikubwa, nyika za ukiwa na majangwa ya kiu. Alivuka mitoni na pengine aliabiri vyomboni katika maziwa na bahari. Kwa tabia ya kiungwana, ambayo msafiri huyu alikuwa nayo, watu aliokutana nao safarini walimwajabia; na kwa ulimi wa adabu, ambao ni azali ya utu wema, alifanya marafiki waliomsaidia katika shida. Kila msafiri ni ndugu kwa wasafiri wengine, lakini yeye alipata ndugu, marafiki na wasaidizi.

"Kila alipokutana na shida, ndipo bidii yake ilipozidi kukua. Baadhi ya watu hulegea mioyo mbele ya dhiki, lakini wengine hukazana mpaka wameishinda. Bidii ya Buruhani ilifanya mwangaza kama wa taa mbele yake, akazidi kupanua hatua kufululiza katika kazi aliyotumwa kwa uthabiti na furaha kubwa. Mwana mwema huyu, msafiri hodari na mjumbe wa kujivuniwa na Kusadikika nzima, aliondoka hapa alipokuwa kijana. Aliporudi kwao alikuwa mzee aliyeyaonja mashaka na mabadiliko mbalimbali. Alijaribiwa na kila taabu, akashawishiwa na anasa zilizo ngumu kuzuilika. Hakusita kwenda mbele kwa uchungu wa shida wala hakughairi kurudi kwao kwa tamu ya anasa."

"Marejeo ya Buruhani yalizibua masikio ya Kusadikika.

Ilikuwa ni mara ya kwanza katika maisha ya wasadikika kusikia kuwa katika nchi ya kaskazini watu wamesitawi sana kuliko wao

Waliambiwa habari za miji mikubwa na majengo ya aushi; mabarabara yaliyosakafiwa na madaraja ya ajabu; utabibu wa watu na wa wanyama; ukulima, mbolea na hifadhi ya udongo; na kuwa wafugaji walikuwa hawashirikiani nyumba zao na wanyama waliowafuga. Ilisemwa vilevile kuwa maendeleo hayo na mengine yalipatikana kwa ushirika wa kazi za watu wote kama mtu mmoja, na fedha yao yote kama hazina moja."

"Rai ya Buruhani ilikuwa kukutanisha bidii za taifa la kusadikika katika shabaha moja. Alitaka maendeleo ya nchi yachangiwe na kila mtu kwa

ushirika wa wazi, fikira na mali. Ushirika huu ulikusudiwa kuendelea mpaka Kusadikika isitawi kama nchi nyingine zilivyositawi na zitakavyokuwa baadaye. Shauri hili lilipowekwa mbele ya serikali ya Kusadikika, ili kuzungumzwa, halikukubaliwa. Natumaini kuwa nikiisha kusema, mtaamua vema kama Kusadikika haikupotelewa na bahati bora shauri hili lilipokataliwa."

"Kwa habari za miji mikubwa ilisemwa kuwa vibanda katika vijiji mbalimbali vikikusanywa pamoja vitatosha kuwa miji mikubwa. Juu ya majengo ya aushi, ilihesabiwa kuwa maisha ya mtu ni mafupi, kwa hivi, majengo ya aushi yalikuwa kazi ya bure. Kwa kuwa unyayo wa mtu hauzidi urefu wa inchi kumi na mbili wala upana wa inchi sita, ilifikiriwa kwamba ilikuwa ni hasara tupu kutengeneza barabara na daraja. Njia yoyote ya desturi ilitosha kwa safari ya mtu. Maradhi yalidhaniwa kuwa kama matokeo ya kuja na kuondoka yenyewe bila ya msaada wa tabibu.

Ukulima ulionekana hauna haja ya kusitawishwa wala kuhifadhiwa; na kuwa mfugaji mwema hasiti kushirikiana nyumba moja na wanyama wake. Fikira za washauri hawa zilikuwa hazifanani na kitu chochote chema katika dunia. Ujinga wao haukuyazuia maendeleo tu lakini hasa ulirudisha nchi nyuma vilevile."

"Kwa kukosekana miji safi, maisha ya Kusadikika yanachukiza. Jengo la kitambo linalopendwa lina gharama kubwa sana kuliko jengo la aushi lililokataliwa. Kibanda hutaka kutengenezwa siku zote. Mtu akiishi umri wa miaka mia moja itampasa kukitengeneza kibanda chake karibu kila mwaka mmoja. Gharama na kazi za jengo hili huanza kidogo lakini huzidi kuwa kubwa kila wakati. Jengo la aushi lina gharama na kazi kubwa pia; lakini baada ya kukamilika, gharama wala kazi hizo haikaririwi mara kwa mara."

"Uchache wa njia nzuri huchelewesha mwendo na hufanya uchukuzi wa bidhaa kuwa mzito. Hapana kitu kijacho wala kiendacho popote kwa upesi kama itakiwavyo. Hata kama nchi ina mazao namna gani, lakini kama haina njia ya kuyapelekea Mazao yake katika soko kubwa, faida haipatikani hata kidogo. Kwa kukosekana kwa madaraja, mito inafanya shida juu ya watu walio ng'ambo moja kukutana na walio ng'ambo nyingine."

“Maradhi hayajapata uuguzaji wa kutosha. Vifo vya mapema hapa katika mwaka mmoja jumla yake yatisha sana kuliko ile ya vifo vitokeavyo katika nchi nyingine katika karne moja. Fikirini kama maisha kama haya yanavumilika au hayavumiliki; na kama hatari hii ya maangamizi ya watu kabla ya wakati wao hayalazimu kuzuiwa kwa bidii yote aliyonayo mwanadamu. Katika amani watu hawatazamii kuchukuliwa na mauti kwa wingi kama katika baa la vita.”

“Kilimo ni uti wa mgongo wa maisha ya mwanadamu. Bila ya kilimo maisha hayawezi kudumu. Nchi hii yaonekana kama imesahau umuhimu wa kazi hii. Udongo usipohifadhiwa, hupotelewa na rutuba yake kila mwaka; na mara kwa mara njaa kali hutokea. Njaa hiyo hufanyiza madhara makubwa sana katika maisha ya watu wanaoishi juu ya udongo uliochujuka. Kama inatazamiwa kuwa watu huweza kuishi kwa nyama, samaki na ndege, lazima ikumbukwe vilevile kuwa hata kuwako kwa vitu hivi hutegemea mimea ya nchi. Udongo wa nchi ndiyo hazina bora ya watu.”

“Kwa kazi zake bora na uaminifu mwingi, Buruhani hakushukuriwa ila kuvunjiwa kadiri. Aliabishwa kuwa alileta uzushi uliokuwa hauna faida katika nchi. Zaidi ya hayo, alitumbukizwa katika kifungo cha maisha. Moyo wa nani usiohuzunika kwa msiba kama huu!”

# MJUMBE WA MASHARIKI

Habari ya mashtaka ya Karama ilikuwa imeanza kuenea mjini. Karama alikuwa si mtu maarufu wa kuvuta usikizi wa umati katika mji, lakini umaarufu wa mashtaka yake uliyavuta masikio ya watu sasa. Kila mtu aliyepata kuisikia habari hii alifanya wasiwasi mwingi. Katika siku ya pili, mfalme na madiwani wake walipokuwa barazani, theluthi moja ya wasadikika ilihudhuria vilevile. Watu hawa walitaka kuitazama kesi hii kwa macho na kuisikiliza kwa masikio yao wenyewe. Mbele ya hadhara hii Karama alisema hivi, “ingawa haja ya Kusadikika haikufaulu mara ya kwanza, ujumbe mwingine ulitakiwa. Haja isiyoridhishwa husumbua fikira kama kiu isiyozimwa isumbuavyo koo siku zote. Fikira ya maendeleo ilikuwa imeanza kupambazuka juu ya Kusadikika. Kama jaribu la kuikuza mpaka mavuno yake mema yakavunwa lilikuwa gumu, jaribu la kuiviza halikushawishi bidii za watu vilevile. Labda itaamuliwa vema baadaye kweli iliyomo katika kusema kuwa mwongozo mwema hauwezekani kuvizwa na kitu chochote kibaya mpaka haja zake zitimu. Kusadikika imo katika hali ya pingamizi kubwa. Pingamizi nyingi ziliwakabili watu wa mataifa mengine zamani.

Lakini ushindi uliopatikana mwisho ulibadili misiba yao kuwa fahari ya milele.”

“Mtu mwenye sifa njema alitakiwa kujitolea mwenyewe kwa ujumbe wa mashariki kama mara ya kwanza, lakini sasa mtu kama huyo alipatikana upesi sana kuliko ilivyokuwa ikitazamiwa. Mtu huyo alikuwa akijulikana kwa jina la Fadhili. Habari ya msiba wa Buruhani ilikuwa ikijulikana na Fadhili lakini haikuvunja moyo wake.

Labda ni kweli kuwa mashaka ni mbegu ya uimara katika mioyo ya wanadamu. Kwa mbegu hii ushindi wao humea siku zote mahali palipoangushwa chini na majaribu mazito. Ni fahari iliyoje kwa wanadamu kutumaini kuwa bidii zao ndogo huchipuka ili kuyashambulia tena majaribu mpaka yameshindwa kabisa!

“Nchi za mashariki, kama zijulikanavyo, ziko ng’ambo ya matlai na bahari zilizo pana sana. Fadhili ilimpasa kuabiri na kujihaulisha katika vyombo mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, aliingia katika bandari kadha wa kadha. Safari yake ilichukua miaka mingi ya majaribu magumu. Walakini alikuwa ni mvumilivu wa ajabu. Uvumilivu wake ulikuwa hauna mwisho. Labda kwa kufadhiliwa kipawa hiki kwa kwa wingi, ndipo alipoitwa Fadhili. Usiri wa marejeo yake ulikuwa wasiwasi mkubwa kwa sababu habari zake zilikoma kupatikana kwa muda mrefu. Tumaini la marejeo yake lilipokaribia kukatika na kuhesabiwa kuwa amepotea, Fadhili alirudi kwa ghafla.”

“Habari aliyorudi nayo mjumbe huyu ilikuwa sawa kabisa na elimu. Alizieleza tawala mbalimbali za nchi za mashariki kwa uwazi uliojaa ufasaha na mifano inayojulikana sana. Aliitenda kazi hii kwa wepesi uliowashangaza wasikilizaji wake. Baadhi ya watu waliopata kuyasikia maelezo ya Fadhili wasema kuwa sauti yake bado hawajaisahau. Kwa muhtasari alisema kuwa katika nchi za mashariki, kengele ya mauti ya uchokozi na vita kati ya wanadamu, nchi kwa nchi, au taifa kwa taifa imeanza kulia zamani sana. Bidii kubwa zilikuwa zikifanyizwa za kuyazika mambo haya mawili katika kaburi la sahau.”

“Karibu watu wote walichukia uchokozi kama aibu kubwa, na waliviapiza vita kama laana ipitayo kiasi kwa viumbe waliojaliwa busara ya haki; moyo wa wema; ulimi wa nasaha; masikio ya kusikilizana; macho ya uongozi; pua ya kutambua harufu; ushirika wa amani; ajali moja na Mungu mmoja. Hapana kabisa kitu hata kimoja katika hivi kilichopewa mtu kwaajili ya uharabu. Siasa kubwa huko ilikuwa ni kuwaunganisha watu wote katika urafiki. Juu ya urafiki huo amani ya ulimwengu imekusudiwa kujengwa.”

“Neno ‘uadui’ na mengine mabaya kama yajulikanavyo, watu walikusudia kujaribu kuyatoa katika lugha na kuyafuta katika vitabu. Kwa amri ya serikali matangazo yalienezwa juu ya njia panda, barabara kuu, na kila mahali pa mikutano ya watu ili kuzuia matumizi ya maneno hayo. Imekwisha thibitishwa huko kuwa kama kama kwa vita mshindwa hupata hasara; mshindi kadhalika huandamwa na kisasi cha milele. Hapana mtu

yeyote mwema apendaye hasara ya kushindwa wala kisasi cha ushindi katika maisha yake."

"Mafunzo yote katika nchi hizo yaliambatanishwa na siasa hii. Katika vyuo, watoto walikuwa wakijifunza taaluma ya kufanyiza urafiki mkubwa ambao mwanadamu aliupoteza mwenyewe; lakini baada ya kuliona kosa lake, sasa amejifunga kwa kuutafuta tena. Watoto wote walikua pamoja kwa upole kama wa kondoo. Utaratibu mwingine, kama mtaalamu akikaa na mjinga; wa kwanza lazima amshirikishe wa pili katika elimu; na kama tajiri akikaa na maskini; wa kwanza afanye awezavyo kwa kumsaidia wa pili kwa utajiri wake, ulikuwa katika orodha ya mafunzo katika vyuo vingine. Kwa mambo kama hayo, Fadhili aliona kuwa zawadi kubwa ilikuwa njiani inawajia watu wa mashariki. Alitaka wasadikika waijue habari hii."

"Matokeo ya ujumbe huu yalipowekwa barazani kufikiriwa, badala ya kushangiliwa, Fadhili alizomewa vibaya kabisa.

Lahaula!

Aliitwa mwongo, mwoga na mwotaji wa ndoto zisizotabirika. Fadhili alidharauliwa kwa dharau ishindayo kupakwa tope usoni, kazi yake ilithaminiwa kwamba ilikuwa bure ghali. Maskini huyu alikuwa mtu madhubuti, ama sivyo moyo wake ungalipasuka kwa kuona kuwa jina lake limepotea, na kazi yake haikuthaminiwa kamwe ilivyostahili. Kwa shauku ya uchokozi na kumwaga damu bure, ilisemwa kuwa Kusadikika haikufikiri kwamba ilikuwa ni vema kuutupa ushujaa wake hata kidogo, ili kulifuata shauri la mjumbe ambaye hakuifanyiza kazi yake barabara."

"Ushujaa ni husuni kubwa na hazina bora ya kudumishwa.

Ushujaa kwa mtu ni ngao, kwa nchi ni tegemeo, na kwa taifa ni uwezo. Jambo hili hukubalika bila ya swali. Lakini ziko namna mbili za ushujaa ambazo hazina budi kufikiriwa mbalimbali siyo pamoja. Namna ya kwanza ni ushujaa wa nguvu na silaha, na namna ya pili ni ushujaa wa kweli na nasaha. Kwa ushujaa wa kwanza wanadamu huipata amani ya kitambo na fahari ya kifauongo-ule mmea usiohimili kuguswa-lakini hufuatwa na vita mara kwa mara. Kwa ushujaa wa pili yafikiriwa kwa sababu bora kabisa kuwa wanadamu wataipata amani ya daima."

“Kusadikika imekwisha pigana vita vingi. Katika kila kitali cha vita imejipambanua kwa ushujaa, lakini kwa ushahidi ulio wazi imepigana punde kwa punde na adui yule yule aliyeshindwa zamani, ndugu yake, mtoto wake au mjukuu wake. Mwendo umekuwa huu na utaendelea kuwa vivi hivi siku zote kwa sababu-ushindi wa nguvu hauwezi kusuluhisha mioyo ya wanadamu ila kuivimbisha kwa kisasi. Inastaajabisha kwa nini dunia haitumii alili nyingi kwa kuijenga amani ya daima badala ya kuitumia nguvu nyingi kwa kuitafuta amani ya kitambo tu. Fadhili alikuwa katika wazo la kuwa njia ya kwanza huwagharimu watu hasara kubwa sana kuliko gharama ya njia ya pili. Hitilafu iliyopo kati ya njia hizi mbili haitaki maizi tu kuigundua. Hata mtu yeyote aliye mwema aweza kuiona faida ya njia ya pili na hasara ya njia ya kwanza.”

“Wa aidha, hata kama matokeo ya ujumbe wa mashariki yalibuniwa kama walivyodai washauri wa serikali, lakini yalikuwa si mabaya kamwe. Yalibuniwa kwa njia inayowezekana kutendwa na watu kwa faida ya maisha yao na Kusadikika nzima. Izara na kifungo zilikuwa ni tuzo njema kwa Fadhili. Uko wapi uso usiotahayari kwa aibu kama hii!”.

# MJUMBE WA KUSINI

Karibu masikio ya watu wa mahali pengi yalijaa habari za Karama na mashtaka yake. Umaarufu wake wa ghafla ulizungumzwa karibu na mbali. Mtu yeyote wa desturi anapozuka katika umaarufu, huyavuta masikio na macho ya watu wengi kwa sababu jambo kama hili hutokea kwa nadra sana kwa watu ambao bahati mbaya imeshughulika kuwaweka nyuma. Kwa hivyo, katika siku ya tatu baraza ilihudhuriwa na mfalme, watu wenye vyeo mbalimbali, pamoja na nusu ya umati mkubwa wa Kusadikika. Fikira zilizochanganyika ziliushika umati huu. Baadhi ya watu walimwajabia Karama, wakamhesabu kama bora wa karne yao. Hawa walitumaini kuwa ataokoka. Lakini watu wengine waliwaza kuwa Karama alikuwa kama mjinga aliyekuwa akicheza na hatari kubwa iliyofunua taya mbele yake. Waliokuwa wakimtazamia kuokoka walikuwa na wasiwasi wao ; na wale waliokuwa wakimtazamia kuanguka walikuwa na fadhaa yao. Walakini hapana mtu hata mmoja aliyepata kulisema wazo lake. Bila kujua alivyoajabiwa wala alivyodunishwa Karama aliendelea kusema mbele ya baraza, “watu wanaoteswa ndio wanaoyajua kabisa mateso makubwa sana. Maisha yaliyozungukwa na maradhi na mauti, uadui usiokwisha, nchi iliyokaribia kugeuka jangwa na mwamba, na madhila mengine mazito yaliyowakabili watu. Walitaka faraja katika mateso haya. Jitihadi baada ya jitihadi ilijaribiwa ili kuiharakisha saa ya maendeleo ya nchi, lakini mara kwa mara majira yake yalirudishwa nyuma. Kama hili lilifanywa kwa makosa au makusudi ni siri iliyo ng’ambo ya fahamu yangu hata sasa. Lakini kama siri njema kufichuka, ile iliyo mbaya haifichiki hata kidogo. Uchaguzi wa wajumbe ulikuwako lakini mathibitisho ya matokeo ya ujumbe hayakupatikana. Kusadikika iliishi kuona mjumbe baada ya mjumbe kuadhiriwa na kuadhibiwa vibaya. Kama washauri hawakudhuriwa na hili, watu wengine walidhuriwa sana. Kazi njema za wajumbe wawili zilipotea bure. Manung’uniko ya lawama hili yalikuwa katika hewa yote ya Kusadikika. Hili lilipotokea, serikali iliombwa ima fa ima kufanya ujumbe mwingine. Basi mjumbe wa tatu alitakikana ajitolee mwenyewe kwa ujumbe wa kusini.

“Wito wa mjumbe wa tatu uliitikiwa na Kabuli, mtu mwenye busara, haya na mcheshi. Yeye alipatikana upesi kabisa kuliko ilivyokuwa katika mara mbili zote zilizotangulia. Misiba ya Buruhani na Fadhili ilikuwa mikubwa ya kutosha kuikongoa mioyo ya bidii katika bawaba zake. Kabuli aliyajua haya yote lakini alikuwa mtu mwenye moyo wa namna nyingine kabisa. Alikuwa na bidii kubwa kama ile ya siafu athubutuye kukivuka kijito kwa daraja iliyofanywa kwa maiti ya siafu wengine walioelea majini huko na huko. Maji yalijulikana kuwa ni

asili ya rutuba, mvuke na umeme. Nguvu nyingine za namna mbalimbali zimo pia katika maji. Kama siafu, mdudu mdogo na kipofu, wakati mwingine haogopi kuzikabili nguvu hizo pamoja na hatari zake kwa sababu njema, basi ni dhahiri kuwa viongozi wa wanadamu wanapoteswa bure, bidii za wafuasi wao hutanuka ajabu. Hapana tisho liwezalo kuukomesha mwendo huu. Kwa hakika utafululiza kuwako duniani mpaka mateso yakome kabisa, na labda wakati huo dunia hii itakuwa njema kama itamaniwavyo kuwa. Buruhani na Fadhili walitoa sadaka zao bora ili kuyahimiza majilio ya wakati uliotakikana sana. Kabuli aliwaona watu wawili hawa kama wafadhili wakubwa wa ulimwengu. Alitaka kuwa mshirika wao kwa thamani yoyote ya maisha yake.”

“Kama ijulikanavyo, kusini ni upande wa dunia yatokako matufani makubwa na baridi kali sana. Kabuli aliyakabili mashaka hayo bila ya kigeugeu. Naam, alikuwa kama mtu aliyekuwa akinywa uchungu mwingi bila ya kigegezi. Mara mbili alikamatwa akafanywa mahabusu. Mara ya kwanza alikamatwa Juju, nchi ya mfalme Jeta. Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijulikanacho duniani kilikuwa laini kama mkate kati ya meno ya majuju; na kilicho kichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Kwa ulafi uliokithiri viumbe hawa, walikuwa hawajui halali wala haramu. Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako midomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana.

Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni moja za mwamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo, na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani pia kila dakika tano. Lakini kila dakika moja Jeta alilia: ‘Kiu,

njaa, kiu, njaa! Mfalme alitaka kumla Kabuli bila kugawana na wawindaji waliomkamata. Choyo chake kikubwa kiliwaudhi wawindaji, pakatokea vita baina ya majeshi ya mfalme na raia. Kwa vita hivyo kila kitu kilichokuwa na uhai kiliangamizwa, akabakia Kabuli peke yake. Huu ulikuwa wokovu mwembamba kama unywele."

"Baada ya kushukuru uwezo uliomwokoa, Kabuli aliendelea katika safari yake mpaka akafika Hasira, nchi ya watu wakali kabisa. Huko alikamatwa tena, akashtakiwa kwamba alikuwa mjasusi aliyeingia katika nchi bila ya idhini. Kabuli alijiona kama aliyeokoka katika moto akatumbukia katika bahari. Kitu alichofikiri kumuokoa sasa kilikuwa hati aliyopewa na serikali yake. Aliitoa hati hii ili kujithibitisha kwamba alikuwa msafiri wa amani asiye na hatia, lakini karatasi iliyoandikwa kwa watu waliopofuliwa na hasira ilikuwa kama utusi mtupu. Basi alihukumiwa kwanza, kulichimba kaburi lake mwenyewe; pili likiisha ajilaze mwenyewe juu ya ukingo wake ili afungwe kwa pingu mikononi na miguuni; na tatu, shingo yake ikerezwe kwa msumeno kidogo kidogo mpaka mshipa wa mwisho ukatike ndipo atumbukizwe kaburini na kufukiwa. Ulinzi wa askari wawili wenye silaha ulikuwa juu yake."

"Kabuli alipokuwa akilichimba kaburi lake kwa kisigirima, jembe lililochakaa, ilichimbuka johari kubwa na nzuri sana. Kwa mtu aliyekaribia kumezwa na mauti, johari ni kama jiwe tu. Kabuli hakufikiri kwamba iliweza kuwa rushwa ya wokovu wake hata kidogo."

Adhabu yake ya kwanza ilipokwisha, alitoka nje akawaonyesha askari waliokuwa wakimlinda johari aliyoigundua. Kwa kuona hivi, kila askari aliidai johari ile kuwa yake. Palepale lilitokea pigano kati yao lililowasukuma wote wawili katika kaburi lililokuwa wazi, wakatumbukia ndani yake kwa mshindo mkubwa sana. Mshindo huu uliufanya mchanga wa pande zote nne juu ya kaburi kubomoka na kuwaelemea juu yao. Walikufa wakati uleule. Kwa tokeo hili Kabuli aliokoka pamoja na johari yake. Huu ulikuwa wokovu mwingine wa ajabu sana. Ulafi wa Juju na upofu wa Hasira ni laana tupu. Kabuli hakuvitaka vitu hivi. Alitaka mambo yaliyo bora kwa ajili ya nchi yake. Kwa hivi, baada ya kuokoka alisafiri tena mpaka akafika Kiasi. Hii ni nchi moja katika nchi zilizosifika kwa usitawi na maendeleo bora kabisa. Wakiasi walikuwa na fahari kubwa sana

katika dunia. Waliheshimiwa na mataifa mengine kwa sababu walikuwa na kiasi, wastani, kadiri na mpaka katika matendo yao yote. Kabuli aliiajabia sana nchi hiyo, akajifunza yote aliyoyaweza kwa ajili ya kusadikika.

"Zamani za marejeo yake hapa, alisema habari za mamlaka ya kiasi, heshima iliyo na wastani, uhuru wa kadiri, na nguvu yenye mpaka. Mtu mwenye mamlaka ya kiasi hawatesi watu walio chini ya mamlaka yake wala hajitesi yeye mwenyewe; mwenye heshima iliyo na wastani hujiheshimu yeye mwenyewe na wengine; mwenye uhuru wa kadiri ni muungwana yeye mwenyewe na wengine; na mwenye nguvu yenye mpaka hadhulumu wala yeye hadhulumiwi. Mambo manne haya ni mbegu za mimea ya mazao ya hali njema, mapatano, ustawi na amani duniani. Mbegu hizi zililetwa hapa kutoka mbali kwa kusudi la kupandwa katika ardhi ya Kusadikika. Kwa kupandwa katika ardhi ilikusudiwa kuwa mambo haya yakizoezwa katika mioyo ya watu matokeo mfawadha yatakuwako katika maisha yao. Kabuli hakutazamia kuwa watu watafaidiwa na mazao yake tu, lakini alitumaini vilevile kuwa chini ya kivuli cha matawi ya mimea hii watesaji na wateswa watapumzika na watakane nasaha kwa mapenzi na furaha."

"Kiasi katika matendo huwapa watu maisha yasiyo wasiwasi. Dunia yao ya ajabu, kwa desturi, imejigawa katika viasi vingi sana. Ina mchana wa nuru na usiku wa giza, hari na baridi, na mengine mengi. Hapana mfalme awezaye kudai kuwa mchana ni wake peke yake, wala raia mwenye haki ya kusema kuwa usiku ni wake peke yake. Vitu hivi ni milki za watu wote. Kama mchana na hari vingefululiza kuwako bila ya kiasi maisha yangechujuka na kuyabisika; na kama usiku na baridi vingefululiza kuwako bila ya mpaka, maisha yangevia na kuganda. Basi kama wanadamu wana tabia ya kunung'unika mara kwa mara juu ya hari nyingi au juu ya baridi kali-mambo yanayotokea kwa kudura-hapana shaka kuwa wana haki pia ya kunung'unika juu ya mamlaka yasiyo kiasi, heshima isiyo wastani, uhuru usio kadiri, na nguvu isiyo mpaka. Si halali mwenye mamlaka kuyatumia ovyo; ni haramu mheshimiwa kuwavunjia wengine heshima zao; hakuna uhuru wa matendo maovu; ni lawama kutumia nguvu tupu. Kwa kila hali mafunzo ya Kabuli yalikuwa si mabaya. Hata kama kitu ni bora kama nini, kama hakina kiasi ni dhara kubwa. Walakini ijara ya Kabuli kwa kulithibitisha neno hili ilikuwa kunyang'anywa johari iliyomwokoa,

kifungo na kazi ngumu katika giza la usiku wa manane. Macho gani yasiyolengalenga machozi kwa ubaya kama huu.”

# MJUMBE WA MAGHARIBI

Habari za Karama zilifanya maenezi makubwa sana. Kwa muda mfupi, toka zilipotokea, zilizungumzwa mahali pengi na watu kadha wa kadha, zikamsisimua kila mtu aliyezisikia. Sasa watu waliokuwa wamezisikia walikuwa wengi sana kuliko waliokuwa bado kuzipata. Basi katika siku ya nne, baraza lilipofunguliwa, alikuwapo mfalme pamoja na theluthi mbili za halaiki kubwa ya Kusadikika. Eneo lote la baraza lililokuwa kubwa kabisa katika baraza zote za dunia liligharikishwa na watu na umati wa watu waliokaa kitako vitini, waliosimama wima, na waliochuchumaa nyuma ya watu wengine ili kumsikiliza na kumtazama mshtakiwa. Jozi za macho ya watazamaji zilimtazama bila ya kupepesa, na jozi za masikio yao zikamsikiliza kwa makini mengi. Palikuwa hapana nafasi tupu wala dirisha lililokuwa halichunguliwi. Watu walijaa pomoni pande zote. Walijaa upande wa kulia na wa kushoto, mbele na nyuma, na karibu hewa yote ilikuwa moto kama tanuu kwa pumzi.

Mbele ya umati huu Karama alitamka, "baada ya kutenda yote waliyoweza kwa ajili ya nchi yao Buruhani aliponzeka, Kabuli alihusudika, na Fadhili akateswa mateso makubwa. Zawadi walizotunukiwa na nchi waliyoipenda zilikuwa ghera na adhabu tupu. Ingawa watu hawa wangali hai hata sasa, lakini wake wao wamekwisha onja eda chungu, na watoto wao wamepatwa na uyatima wa kusikitisha. Dhiki za nchi na misiba ya watu hawa, ikiwekwa pamoja, hutosha kuifanya jumla ya mashaka ya kusadikika kuwa kama nusu moja ya mashaka ya dunia nzima. Nchi moja yoyote ikipatwa na nusu moja ya mashaka ya dunia nzima ni mateso yaliyo makubwa kabisa. Haiyamkiniki kuwa wako watu mahali popote wapendeleao kufululiza kushinda mchana kutwa na kulala usiku kucha juu ya miiba ya mashaka ya dunia."

"Lila na Fila hawatangamani. Kinywa cha Lila kikisema, sikio la Fila hujidai halisikii; jicho la Lila likiona, lile la Fila hujifanya halioni; moyo wa Lila ukijilainisha kwa mapenzi na huruma, ule wa Fila hujifanya mgumu kama jiwe lisilo maisha kwa chuki na uadui."

Watu wa Kusadikika na washauri wao wameishi katika hali kama hii kwa muda mrefu sana. Kwa bahati mbaya, Fila na watu wake wachache iliyashika mamlaka ya Kusadikika, lakini kwa bahati njema, Lila na watu wake wengi ilikuwa chini ya mamlaka haya. Waovu wachache hawawashindi wema wengi. Kwa kuwa hapana sikio gumu duniani lisilosikia vinywa vingi vikisema kwa umoja, ombi la kuchagua mjumbe wa nne kwa safari ya magharibi lilipofanywa lilikubaliwa. Kwa washauri waliokuwa vipofu wa heri na shari yao, wajinga wa salama na maangamizi yao, na waliokuwa wamejifunga kukipinga kitu chochote kigeni au kisichofikiriwa na wao wenyewe, kukubaliwa kwa ombi hili ilikuwa takilifu kubwa sana kwao. Walitazamia kuwa mtu mwingine hatapatikana kwa ujumbe huu lakini alipatikana mara moja.

“Mtu aliyejitolea mwenyewe kwa ujumbe wa magharibi aliitwa Auni. Auni alijua kuwa kazi za watangulizi wake ziliishia katika mto wa jangwani unaoyapoteza maji yake bure, lakini hakulegea. Kwa hakika, mtu huyu alikuwa na bidii ya mchwa ya kujenga nyumba kwa mate. Watu walio kama Auni ni wafadhili wakubwa wa dunia. Fadhili zao ni deni kubwa sana lisilowezekana kulipika lote. Kila jitihadi ya kulilipa deni hilo hulipunguza tu lakini halililipiki. Kwa hivi mtu yeyote anayeyakabili mashaka bila ya kutetemeka hata kama hadiriki kuyashinda kama atakavyo huishi maisha mema, mtu yeyote anayeyakabili mashaka , akayashinda nusu, huishi maisha bora, na anayeyakabili mpaka akayashinda yote, huishi maisha bora kabisa. Na mtu yeyote anayeyapa mgongo, akayaonyesha visigino mashaka yanayostahili kushindwa-kama kuishinda njaa kwa kilimo; kiu kwa visima, mifereji, au mabomba; umaskini kwa kazi; maradhi kwa utabibu, na mengine-ni duni sana kuliko mnyama au mdudu. Kama ni karaha kumlinganisha mwanadamu na mnyama au mdudu mwenye sifa mbaya, basi ni fahari pia mtu kulinganishwa na mnyama au mdudu mwenye sifa njema kama mchwa na wengine.

“Magharibi ni machweo ya jua na mwezi. Pia ni upande wa dunia wenye giza limezalo nuru zote na ufupishao uoni wa macho. Auni aliyakabili mashaka haya akafanya safari kubwa sana. Baada ya miezi mingi kupita, siku moja alikutana na vipofu wawili njiani. Vipofu hawa wote walikuwa wanaume. Kipofu mmoja mbele na wa pili nyuma. Uso wa kipofu wa kwanza ulikuwa na furaha kama uso wa bwana harusi, akaonekana kama

aliyeridhika kabisa. Lakini uso wa kipofu wa pili ulikuwa umeghadhabika na kinywa chake kilijaa manung'uniko mengi kama aliyekuwa hakuridhika hata kidogo. Kila hatua aliyokwenda alibwata akailaani bahati yake. Auni alishangaa sana kuona vile, akasema moyoni mwake kuwa watu hawa wana vilema namna moja, lakini mmoja amekinai na mwingine hakukinai. Ajabu kubwa ilioje hii! Afadhali niulize ili nielewe sababu zake. Baada ya kukusudia hivyo alitamka, 'mabwana, nyinyi ni kina nani, na asili ya upofu wenu ni nini?"

"Kipofu wa pili alijibu, 'bwana wangu mwema, mimi naitwa Sapa na mwenzangu Salihi. Salihi haombi neno akalikosa. Ameishi maisha haya tangu ujana wake, lakini vitu alivyopata kwa maombi aliyoyafanya alikuwa hana matumizi navyo. Nilipoona hivyo nilimwambia kuwa niliota ndoto kuwa akiomba kitu chochote tena bila ya kugawana na mimi sawasawa, dua lake halitapokewa hata kidogo. Kwa sababu hii tuliafikiana kushirikiana kila kitu atakachokiomba tukaandikiana hati mbele ya kadhi. Hati ya mkataba wetu ilipokwisha andikwa nilifurahi sana kuwa shauri langu limefaulu, lakini palepale mwenzangu aliinua mikono yake juu akaomba upofu, na kabla sijatanabahi, sisi sote wawili tulikuwa vipofu. Kama yeye anaipenda hali hii, mimi naichukia kabisa. Nilidhani ataomba niwe mfalme nizungukwe na mawaziri na kuheshimiwa na raia, au niwe tajiri ili niwatumie maskini kama nguo mbovu. Fahari ya mambo haya ndiyo iliyonishawishi kufanyiza mkataba na Salihi. Kama angalikataa kushirikiana na mimi katika fahari hii, pasingalikuwa na dawa yoyote kwa sababu nilimdhihaki tu. Sina haja ya upofu huu. Nimemnasihi sana aombe nirudi katika hali yangu ya zamani lakini hakubali. Tafadhali nisaidie kumnasihi, bwana."

"Kabla Auni hajalijua neno la kutumia, Salihi alisema, 'mimi naapa kuwa sikujua kama Sapa alitamani ufalme au utajiri wakati aliponiagulia ndoto yake. Laiti ningalijua nia yake ilivyokuwa, hili lisingalitokea. Ningaliomba madua mawili mbalimbali, yaani moja langu na jingine lake na kila mmoja katika sisi angalipata haja yake. Nilipoona mambo ya dunia yamenichukiza, nilidhani kuwa mwenzangu yamemchukiza vilevile, na kwa mujibu wa mapatano yetu nikaomba upofu ili tuishi bila ya kuyaona tena. Madhali neno nililoliomba nimelipata, wajibu wangu sasa ni kushukuru. Haiwezekani kuomba niyaone tena mambo niliyoyakataa. Nikifanya hivyo,

nitafanana na ng'ombe anayeutia ulimi wake puani na kuurudisha tena kinywani. Si laiki ya mwanadamu kuwa kama ng'ombe kwa neno alilolichagua kwa hiari yake mwenyewe.' Basi Auni alimwambia kipofu wa pili, 'pole, Sapa, lakini huna budi kuvumilia mazao ya wivu wako sasa ili ujifunze kuwa bahati ya mwenzio usiilalie nje! Kila mtu ana bahati yake njema."

Auni aliendelea katika safari yake lakini sasa kila hatua aliyokwenda ilimvuta katika giza kuu. Kutahamaki aliteleza na akatumbukia katika mkondo wa mto uliokuwa ukikimbia kwa nguvu na upesi kama umeme. Miongoni mwa vitu vingi vilivyokuwa vikielea katika mkondo huo lilikuwamo gogo moja la wastani. Auni alilishika gogo hilo kwa mikono yake miwili na kichwa chake akakiweka juu ya maji. Karibu mwili wake wote ulikufa ganzi kwa baridi, lakini baridi hiyo iliuzidisha mkazo wa mikono yake juu ya gogo hilo. Alikuwa hajui anachukuliwa wapi. Mapambazuko ya mashariki yalipomulika nuru yake, aliona mto umejigawa mikono miwili. Mkono mmoja ulikuwa unakwenda upande wa kulia na wa pili upande wa kushoto.

Mkondo wa upande wa kulia ulikuwa umeinuka juu kama mlima mkubwa, akausikia mshindo wa maanguko makubwa kabisa ya maji. Upande wa kushoto ulikuwa hauna mwinuko. Kabla ya kufika njia panda ya mkondo huo aliukingamisha mguu wake wa kushoto majini kama usukani wa chombo. Aliyafumba macho yake ili asijione jinsi atakavyovunjwavunjwa katika maanguko ya maji ya upande wa kulia kama gogo lake halikufaulu kwenda upande wa kushoto. Kwa bahati njema, gogo lake lilifaulu kuelea katika mkondo wa upande wa kushoto, likaingia katika kuko(bomba la maji kubwa sana) lililokuwa na maji yaliyo shwari. Auni alikuwa bado amelishikilia gogo lake lakini hali yake sasa ilikuwa taabani. Alikuwa hajijui mkono wala mguu. Aliopolewa katika maji akasaidiwa na watu wema waliokuwa juu ya kuko. Fahamu ilipomjia lakini bado macho yake ameyafumba, na mwili wake wote umefunikwa kwa blanketi na kuegemezwa juu ya mito kichwani na mbavuni alisema kwa sauti hafifu sana, 'niko wapi?'

Alijibiwa, 'hapa ni Iktisadi, nchi ya utajiri na faraja kwa kila mtu. Fumbua macho yako utazame. Ulitumbukia katika maangamizi ya

matumizi, yaani mto mmoja katika mito ya uharibifu mkubwa na yenye nguvu nyingi kabisa duniani. Maisha ya watu wengi sana yametota katika mto huu. Mahali ulipoteleza ukatumbukia majini mpaka hapa ni mwendo wa miaka kumi kwa miguu. Kwa nguvu ya mkondo wa mto uliotumbukia ndani yake umefika hapa kwa muda wa saa kumi, kila mwaka mmoja kwa saa moja tu. Watu watumiao mali zao kwa ubadhirifu husemwa kuwa wametumbukia katika maangamizi ya matumizi.

Mwisho wa watu hao huvunjwavunjwa katika maanguko ya umaskini, yaani, njaa, kiu na uchi. Watu watumiao mali zao kwa uangalifu huyaepa maanguko ya umaskini kama wewe ulivyookoka kutota katika maanguko ya mto huu. Kwa kuwa watu walio wengi hawaijui hatari ya matumizi yao, Iktisadi imejenga kuko la kuyazuia maji ya mkondo wa kushoto ili kuwaashiria watu hatari ya matumizi mabaya. Tangu kuko hili lisimame maisha mengi yameokolewa.

Kwa hivi mfano mwema umepatikana kuwa nguvu ya matumizi mabaya huwezekana kuzuilika kwa Iktisadi kama mkondo wa maji haya ulivyozuilika kwa kuko hili. Hazina kubwa hufanywa kwa kukusanya senti mojamoja kama safari ndefu ifanywavyo kwa mwendo wa hatua moja moja. Tumekuja duniani kutafuta hazina bora na kusafiri safari kubwa kwa njia mbalimbali. Ujinga wa matumizi yetu hututenga na hazina zetu, na uvivu wa kunyanyua hatua zetu hutuchelewesha nyuma siku zote. Mtu yeyote asiyelitunza pato lake dogo hawezi kuwa tajiri, na yeyote asiyejali kuenda hatua hatua moja mbele huwa mzigo mzito kwa wasafiri wenziwe. Hapana mtu mwema anayependelea kuwaudhi wengine kwa uzito wake kama anayo njia ya kuupunguza."

"Katika marejeo yake, Auni alisikitika sana juu ya wivu na ubadhirifu mkubwa wa Kusadikika. Alisema kuwa kwa upofu tulio nao, marafiki zetu wema wamekuwa maadui wetu wabaya. Hatuishi kuwabughudhi watu wengine wala sisi hatuishi kubugudhiwa na wao. Hatuwapendi watoto wa wenzetu wala wetu hawapendwi. Nani mwenye haki ya kuchafua maisha ya namna hii katika ulimwengu? Kwa ujinga wa matumizi yetu mali zetu zote huishia katika ngoma na tafrija za kufukarisha. Twaoana kila siku na twaachana kila siku. Mume mmoja ana fedha kiasi gani cha kuwaolea na kuwakimu wanawake wote wazuri, au mke mmoja ana uzuri gani wa

kuolewa na kila mwanamume? Tunazaa watoto wengi lakini hatuwalei kiungwana kwa kuwafunza kuzijua dhima zao katika dunia kwa sababu fedha yote imetupotea.

Kwa mafunzo haya Auni alighadhabikiwa kuwa alileta miujiza isiyofahamika katika nchi ya Kusadikika, akafungwa kama watangulizi wake. Kwa hakika mafunzo ya Auni yalikuwa mema na yaliyoigika lakini yaliangukia katika masikio ya viziwi.

Kusadikika itashukuru lini fadhili za watu wake bora?”

# MJUMBE WA MBINGUNI

Tangu mwanzo wa mashtaka ya Karama watu waliohudhuria barazani hawakuondoka, na kila siku watu wengine walikuja. Kila mtu aliyeisikia habari hii alishika njia kwenda Sadiki. Mamiminiko makubwa ya watu yalimiminika katika baraza ya Sadiki kama mto uliofurika wakati wa masika. Karibu sudusi tano za umati wa Kusadikika zilipata kuhudhuria barazani katika siku ya tano ya kesi hii. Mbele ya umati huu mkubwa Karama aliendelea kusema, "katika kuthibitisha kweli watu hawachelei msiba wowote. Huu ni mwongozo mmoja katika miongozo iliyo bora kabisa kwa wanadamu. kwa mwongozo huu wanadamu ni washindi siku zote juu ya majaribu yao mabaya. Hatuna budi kumshukuru na kumhimidi anayetuongoza hivi mchana na usiku. Karibu madhila ya namna moja yaliwaangukia wanne waliotangulia.

Lakini mjumbe wa tano alipopatikana alitokea bila ya ajizi. Mjumbe huyu alikuwa Ridhaa. Ridhaa alijua matokeo ya kila mjumbe aliyetangulia, lakini matokeo hayo hayakupunguza ukufi katika bidii yake kuu. Mashaka yetu makubwa hushindwa kwa bidii zetu kuu. Mjumbe huyu alisafiri kuelekea mbinguni. Alirudi hapa na ardhilhali iliyo muhimu kabisa. Aliandika kuwa kwa msaada wa malaika aliyeyasimamia mambo ya wanadamu aliweza kufika mpaka halmashauri kubwa za mbinguni. Halmashauri hizo zilikuwa mbili zilizoitwa hifadhi na dhahiri."

"Majengo ya halmashauri hizo yalikuwa ya ajabu kubwa kabisa. Yalijengwa kwa majohari bora na ya namna ya peke yake, yalisakafiwa kwa dhahabu safi tupu. Majohari hayo hayakupatikana mahali popote ulimwenguni. Kila halmashauri ilikuwa juu ya uwanja mpana uliokuwa na mabustani. Mabustani hayo yalivuta sana macho kwa uzuri wa maua yake ya ajabu. Sanamu zilizochorwa kwa majohari mbalimbali zilikuwa zimesimama nje na ndani ya halmashauri hizo. Sanamu za nje zulikuwa za wanaume mashuhuri wa rangi na sura mbalimbali, na zile za ndani zilikuwa za wanawake bora wa mataifa mbalimbali waliojipambanua kwa matendo ya heshima katika maisha yao. Hii ni shani iliyokuwa na uzuri wa mwisho."

“Kwa kulinganisha jumla, Ridhaa aliona kuwa sanamu za wasadikika zilikuwa si nyingi kuliko zile za watu wa kila upepo uliopakana na Kusadikika, yaani wakaskazi, wakusi, wamashariki na wamagharibi. Jumla ya wakaskazi walioheshimiwa kwa sanamu zile karibu ilipita ya wakusi; na idadi ya sanamu za wamagharibi waliotukuzwa kwa sanamu ilikuwa ndogo kuliko ile ya wamashariki. Jumla ya sanamu za watu wa ardhi waliotaadhimiwa kwa sanamu ilionekana kama ilishinda jumla ya sanamu nyingine zote za watu wa pepo nne. Sababu ya hili, mjumbe wetu aliambiwa kuwa majaribu ya watu wa ardhi yalikuwa makubwa sana, na kuwa namna walivyokuwa wakiyashinda kwa matendo yao bora ilistaajabisha kabisa.”

“Matendo ya watu wote walioheshimiwa wa sanamu zile pengine hayakushangiliwa na wenzao duniani kwa sababu yalitendwa faraghani ambako hayakuonekana na wengine. Baadhi ya matendo yalionekana lakini kwa sababu ya ujinga, wivu na dharau hayakushangiliwa vilevile. Matendo hayo hayakusahauliwa. Yalipata shangwe kubwa sana mbinguni, yakafanyiwa makumbusho ya milele. Makumbusho hayo ni ushahidi bora wa watu walioziabisha bidii za shetani na waliothubutu kuupaka uso wake tope na masizi. Haya ni maendeleo makubwa yalioje!”

“Dazani za malaika zilikuwa zikizunguka kwa zamu kando ya sanamu za nje wakaimba kwa sauti nzuri kabisa. Utaratibu huu huu ulizizunguka sanamu za ndani zilizokuwa zikipuliza manukato mazuri kabisa. Mipulizo ya manukato ilipenya madirishani ikaeneza harufu ya kupendeza nje ya halmashauri zote mbili. Maisha yote ya huko yalizungukwa na sauti za kutumbuiza, harufu za kuliwaza na maua ya kupendeza. Nyimbo zilizoimbwa zilikuwa juu ya haki, kweli, wema, mapenzi, imani na bidii. Kila kinywa cha malaika kilishinda kinanda, santuri na zeze. Sauti hizo zilisemwa kuwa ni roho zilizookoka, na kuwa zilikuwa zikimshukuru aliyeziumba na kuisifu miili, zile sanamu, aliyezichukua na kuzilinda vema zilipokuwa katika maisha yake ya kwanza ulimwenguni. Roho hizi zilikuwa tayari kurudi tena katika miili yake. Maisha mapya na ya milele yaliyolipiwa gharama zote kwa matendo mema yalikuwa yanazingojea kwa furaha. Ni hasara kubwa ilioje kwa mtu kuikosa fahari kama hiyo!”

“Katika hifadhi mashauri kadha wa kadha yalizungumzwa kwa siri yakahifadhiwa kwa kuandikwa kwa taratibu nzuri sana. Mashauri yenyewe yalihusiana hasa na maandao ya mambo yaliyonuiwa kutokea au kuwa katika nchi na kwa watu wa mataifa mbalimbali duniani. Yaliweza kubadiliwa na kusahihishwa kwa kadiri iliyofikiriwa na kuonekana ilifaa kabla ya kuafikiwa na halmashauri hii. Katika dhahiri, makusudio yaliyopata mwafaka katika halmashauri ya kwanza yalitangazwa kwa malaika kwa mbiu kubwa kabisa kuwa nchi fulani itakuwa hivi, taifa fulani litakuwa vile, mtu fulani atapata hiki, au fulani atapatwa na kile kwa tarehe na wakati maalumu. Halmashauri ya pili haiamuru badiliko lolote.”

“Halmashauri hizo zililindwa sana ili zisisogelewe na upelelezi wa kiumbe yeyote mwingine ila malaika. Walakini mjumbe wetu alisikia kuwa pengine zilinyemelewa kwa siri na mashetani kwa kusudi la kusikiliza mambo yaliyokuwa yakisemwa huko. Kisha mashetani hao walishuka chini na umbea. Umbea huo ulienezwa Kusadikika na nchi nyingine nyingi na mashetani hao ili kuuthibitisha uwezo wao kwa watu waliowaamuru kuwa walikuwa na nguvu na elimu juu ya mambo yote. Haikudhaniwa kuwa mashetani hao waliweza kupata habari zote, lakini walipata kuokota hapa neno moja na pale maneno mawili au zaidi. Ukufi huo wa habari ulitosha kumwezesha shetani kufanyiza uvumi mkubwa sana kwa wanadamu. Mashetani wambea walipogunduliwa, waliadhibiwa kwa kupigwa kwa nyota, lakini hawakuonekana kuwa walikoma kufanya upelelezi wao. Kwa hivi, si siri za ulimwenguni tu zionekanazo kuvuja toka sikio la mtu mmoja mpaka sikio la mtu mwingine; au toka nchi moja mpaka nchi nyingine kwa upesi wa ajabu kama upepo, lakini hata siri za mbinguni pengine zilivuja chini kama maji zikafika kwa watu kwa sababu ya umbea wa mashetani kama hao.”

“Mashauri makubwa, kama vile vita kati ya mataifa au falme, amani, njaa, maangamizi, neema na mengine katika nchi mbalimbali yalikuwa yakifanyizwa na kukatwa katika halmashauri hizo. Maisha ya watu wa ajabu, kama vile bora kuwa duni, mshindi kuwa mshindwa, duni kuwa bora, na mabadiliko mengine makubwa kama hayo yalitajwa katika halmashauri hizo kuwa yatatokea katika nyakati mbalimbali. Naam, hizo zilikuwa ni halmashauri zilizoongoza mabadiliko makubwa na yaliyo magumu kabisa kutabirika katika maisha ya wanadamu.”

“Katika ardhilhali iliyoandikwa na kuletwa mbele ya madiwani wa kusadikika ili ifikiriwe, mjumbe huyu alitia mkazo mwingi juu ya mabadiliko kuwa yamelazimu kutokea katika maisha kwa jumla ya watu na kwa mtu mmoja mmoja. Kwa kuwa maisha yanaongozwa na utaratibu huu, kazi na hali hubadilika mara kwa mara, na kuwa matendo yetu yote, madogo na makubwa, yana hesabu maalumu mbinguni. Kwa utaratibu huu mkubwa wafalme huvikwa na kuvuliwa mataji yao. Vivi hivi ndivyo baadhi ya watu wapatavyo na waishiwavyo na vyeo vingine vikubwa. Wanadamu hawakuahidiwa aushi katika ulimwengu. Aushi yao haipatikani hapa ila katika maisha ya milele, ambayo hayana budi kuandaliwa vema na kila mtu kwa bidii zote.”

“Alitaka ionekane waziwazi kuwa mapendeleo makubwa hupewa mataifa yatendayo haki, koo zenye wema, na watu mbalimbali wenye adili katika maisha yao. Watu wapatao mapendeleo haya hutasawari katika ulimwengu. Wakikishika kitu kidogo huwa kikubwa kwa bidii zao, haba huwa kingi kwa utunzaji wao mwema, kibaya huwa kizuri kwa kusahihisha kwao; na kwa saburi yao matumaini yao hutimizwa kama walivyoyatazamia ama zaidi.”

“Alitoa hadhari kubwa juu ya uvivu akasisitiza juu ya bidii kuwa ni njia ya kufaulu. Kila jambo lingehesabiwa kama kitabu ambacho kurasa zake zimelazimu kupekuliwa zote kwa uangalifu, kila mstari ndani yake kusomwa taratibu, na kila neno lililomo kufikiriwa kwa makini mpaka maana yake ifahamike waziwazi. Labda nitadhihakiwa na kuzomewa hapa kwa kuwa nayahami mawazo yasiyothibitika. Lakini hata ikiwa hivyo, siwezi kama nitakavyo, kujizuia kusema kuwa ardhilhali ya Ridhaa ilikuwa ni msaada mmoja katika misaada mikubwa kabisa katika bidiii ya maendeleo ya Kusadikika.”

“Wasadikika wana desturi ya kutafuta fimbo baada ya kuumwa na nyoka. Tumekwisha umwa na nyoka wa matendo yetu mabaya ya zamani. Nyoka mwenyewe amekwisha kimbia. Hapatikani kwa kulipiza kisasi, lakini sumu yake imebakia katika jeraha tulilolipata. Sasa shauri lililo jema ni kuizuia sumu hii isienee miilini mwetu ikaleta kifo. Maovu yana hatari kubwa kukaa kati yetu. Tumedumu nayo kwa muda mrefu. Hayakutuletea faida ila hasara, huzuni na kilio siku zote. Lazima sasa yabadilishwe kwa mema ili

Kusadikika isitawi na watu wake wafanywe washiriki katika mapendeleo makubwa na yatamanikayo hapa na mbinguni. Watu wanaojiandaa kwa mapendeleo hayo bidii zao hukutana na ufanisi kabla ya kufika mwisho wa safari yao. Tuna vichwa vya kutuongoza, mikono ya kutendea, na miguu ya kusafiria. Hizi ni zana ali ali kwa matumizi yetu. Uchawi umetembea katika nchi hii ukaizuru kila nyumba ya mtu ili kuviviva vitu hivi?

La, mara nyingi la. Hilo halijatokea wala halitatokea. Basi lazima tuvitumie vitu hivi katika mambo yatakayo bidii kubwa kama tunataka kufanikiwa."

"Wasadikika ni sawasawa na watu wa mataifa mengine, pia ni washiriki katika haki zote kama wangejistahilisha wenyewe kwanza kuwa waweza kuzichukua dhima za mambo hayo. Hili likifanyika heri ingejimimina yenyewe Kusadikika kama mvua wakati wa masika. Kwa nini jambo hili halianzi sasa hivi, linangoja kitu gani? Matendo makubwa huchukua wakati mwingi kukamilika, kwa hivi haifai kuchelewa. Kila dakika moja, na kila nukta moja, ni hazina ; isipite bila ya kutiwa alama kwa tendo jema."

"Lahaula! Inasikitisha kuwa fadhili ya Ridhaa, kwa kuileta Kusadikika habari njema kama hii, ililipwa kwa adhabu vilevile. Alishtakiwa kwamba alikuwa mzushi wa upuuzi wa kuwazuzua watu juu ya maisha ya milele na bidii ikapatilizwa na kifungo. Aliomba rufani juu ya hukumu ya madiwani lakini hakukubaliwa hata kidogo. Mtu hustaajabu kwa nini rufani yake haikukubaliwa kama hukumu hii ilikuwa ya haki! Hakimu gani mwema ayacheleaye macho ya mtu mwingine kutazama hukumu aliyoitangaza kuwa ni haki?"

# MJUMBE WA ARDHI

Siku ya sita iliwakusanya pamoja watu wa kila upande wa nchi ya Kusadikika. Watu wasiohesabika walijaa katika mji wa Sadiki na katika baraza yake. Nafasi ya kutemea mate ilikuwa haipatikani kwa sababu ya umati mkubwa kabisa uliokutana ili kumtazama Karama, mtu mmoja aliyekuwa hajulikani hata kidogo zamani, lakini aliyezuka katika umashuhuri mkubwa sana katika muda wa juma moja tu. Umashuhuri wake ulikuwa kama mbegu iliyopandwa kwa muda wa juma moja yakavunwa mazao yake katika juma ileile.

Siku ya mwisho ilikuwa imefika.

Karama alikuwa akimaliza kutoa maombezi yake. Hakujua kama maombezi yake ya siku tano zilizopita yalimpatia mapendeleo au ghadhabu ya baraza ya Sadiki. Hakujishughulisha kulijua jambo hata moja kati ya mambo mawili haya. Ilikuwa si kazi yake kujua mbele matokeo ya hukumu itakayofanyizwa juu yake. Basi aliposimama alisema.

"Baada ya wajumbe watano kufanyiza kazi zilizowaletea misiba mikubwa, mjumbe wa sita alihitajiwa kwenda katika ardhi. Ilikuwa kama Kusadikika ilitaka kuwapa ujumbe watu wote utakaoishia katika kifungo. Mjumbe aliyepatikana kwa safari hii, labda iliyo ya miujiza mikubwa sana kuliko zile zilizotangulia zote, alikuwa Amini. Amini alishuka katika ardhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa Mangera, ndege wakubwa kabisa waishio katika ardhi lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kwenda chini Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku. Kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini. Alitua ziwani. Nusu ya mapaja yake ilikuwa majini. Kwa hivi Amini alijifungua, akaogelea bila ya kuonekana mpaka ufukoni. Ziwa hilo lilikuwa na maji baridi sana. Amini aliota jua mchana kutwa ili kuondoa mzizimo wa maji hayo. Hali yake ilipokuwa njema tena alizizuru pande zote za Ardhi kama alivyotakiwa na kazi yake. Wakati wa kurudi Kusadikika mjumbe huyu alijifunga tena juu ya paja la Mangera aliyekuwa ameshughulika na kula karamu ya mzoga wa ndovu bila ya kutazama huku

wala huko. Safari hizi zilikuwa za ajabu na hatari kubwa kabisa. Amini hakutambua kama alichukuliwa na ndege mmoja au wawili katika safari hizi mbili."

"Mjumbe wa ardhi aliporudi Kusadikika alinena kuwa wenyeji katika Ardhi walikuwa waadilifu wakubwa kabisa, na kuwa walipasa kuigwa katika bidii zao zote kama Kusadikika ilitakiwa kuendelea katika usitawi. Alitaka sana kuja na mtu mmoja wa Ardhi katika nchi hii. Mtu huyo alikusudiwa kuwa mwalimu hapa lakini haikuwezekana. Lilikuwa sikitiko kubwa kwa mjumbe wetu alipoambiwa kuwa watu wa Ardhi walikuwa hawapai juu mpaka baada ya mauti. Pingamizi hii haikuwapendeza watu wa Ardhi.

Amini alipowaambia kuwa alisafiri kwa Mangera kutoka Kusadikika aliajabiwa sana. Alisifiwa kuwa alifanyiza jambo kubwa kwa usafiri kwa chombo ambacho mwendo wake haukuwa katika uongozi wa kiumbe kama yeye; lakini wao watajaribu kufanyiza jambo lililokubwa sana kuliko lile kwa kusafiri katika hewa kwa chombo, ambacho mwendo wake utakuwa katika uongozi wao wenyewe. Ahadi ilitolewa na watu wa Ardhi kuwa watafanyiza yote waliyoyaweza mpaka pingamizi ya kusafiri katika hewa ishindwe kabisa. Amini aliwaacha katika matengenezo ya chombo cha kuwawezesha kuruka hewani. Wakifanikiwa kutengeneza chombo walichokitaka watakuja huku. Walikwisha faulu kusafiri baharini kwa merikebu, na barani kwa magari. Vyombo hivi viliweza kuchukua bidhaa nyingi nzito mbali kwa muda mfupi sana. Kwa maendeleo haya, Amini aliona dhahiri kuwa watafanikiwa katika matengenezo yao ya kuunda chombo cha kuruka hewani kama walivyokwisha faulu kutengeneza merikebu na magari. Kama mawazo yake yaliongozwa na bidii aliyoiona huko, basi, yalikuwa na msingi mwema. Mawazo ya bidii kubwa ni maendeleo makubwa."

"Mjumbe huyu alishauri Kusadikika kama iliweza kufikiri kutengeneza tayari bandari na viwanja vya kutua vyombo hivyo. Kwa shauri hili, alidhihakiwa kuwa alikuwa kama mama aliyekuwa akimwandalia mtoto aliyekuwa bado kuzaliwa. Ilisadikiwa kuwa watu wa Ardhi walikuwa hawawezi kuvumbua njia ya kuunda chombo cha kusafiria hewani hata kama walifaulu kusafiri baharini na barani. Kwa hivi, Kusadikika ilikuwa

haina haja ya kutengeneza tayari bandari wala viwanja kwa ajili ya vyombo vya ardhi. Andao lolote kwa ajili ya wakati ujao yalikuwa si juu yao, ingawa walijua barabara kuwa watu watakaoishi katika wakati huo walikuwa si wengine ila watoto wao wenyewe. Shauri hili lilikuwa si upuuzi. Lilikuwa ni shauri la hekima sana. Udhahiri wa mambo ni kuwa ulimwengu uliumbwa kabla ya wakaaji wake. Kama ulimwengu usingalitangulia kuumbwa, wakaaji wake wasingalikuwa na mahali pa kukaa. Ukitaka biashara ya vitabu isitawi, watu hawana budi kufunzwa kusoma kwanza. Kusoma kusipotangulia, vitabu vizuri vitaonekana vibaya. Kabla ya kujenga msikiti watu lazima wafunzwe utukufu wa dini mbele. Bila ya hivyo msikiti mtakatifu utakuwa kama mkahawa mchafu tu. Kadhalika mfano, kama nchi haina bandari ya namna yoyote, haiwezi kutazamia kufikiwa na vyombo. Kila azimio katika maisha hutaka neno fulani kufanyizwa mbele ili kuyashawishi maendeleo yake. Watu watakao kusitawi katika maisha huelekeza bidii zao juu ya mshawasha wa makusudi yao kwanza. Kama hii si shabaha ya kwanza katika maisha, basi, haiwi ya pili kwa nyingine yoyote. Mambo yaliyo makubwa na madogo yamefungamana na utaratibu huu."

"Baada ya kudharauliwa kwa shauri la Amini, miaka mingi haikupita ngurumo za vyombo vilivyoonekana vikipita hewani zilisikiwa. Haya yalikuwa mastaajabu makubwa sana hapa. Baadhi ya watu walifikiri kuwa vyombo vile vilitoka mbinguni, na wengine waliona kuwa vilitoka ardhini. Mwisho, watu wote walipatana kuwa vilitoka chini. Kwa namna vilivyokuwa vikipita hewani kwa kusita ilionekana kuwa labda ndani yake walikuwamo watu waliotaka kutimiza ahadi aliyopewa mjumbe wetu, lakini palikuwa hapana bandari wala kiwanja cha kutua juu yake. Majuto makubwa kabisa yaliamshwa. Laiti shauri la Amini lingalishikwa likajaribiwa vyombo vile vingalikuwa vikitua hapa. Abiria ndani yake wangalikuwa wageni wa Kusadikika. Bidhaa zao zingalibadilishwa na zetu. Zaidi ya hayo, Kusadikika ingaliongozwa vema katika usitawi kwa msaada wa watu wa Ardhi. Kwa kulikataa shauri jema katika dakika moja, tumekosa faida ya siku zote. Hasara kubwa ilioje!"

"Kupatikana kwa vyombo vya kusafiria ilikuwa si usitawi peke yake uliofikiwa na watu wa Ardhi. Shauri la ushirika wa watu katika mambo yote lilitiliwa nguvu nyingi sana huko. Kwa shauri hili, ilirazamiwa kuwa

faraka kati ya watu itakoma kabisa. Wataalamu walikuwa na vyuo vya kufunza elimu mbalimbali. Hili liliufukuza ujinga toka kila upande likaieneza elimu kila mahali. Kila mtu alikuwa mshiriki katika elimu. Matajiri waliwafanya maskini waweze kujipatia sehemu katika mali zao. Mashaka ya umaskini yalijulikana na matajiri, na faraja za utajiri zilionjwa na maskini. Bidii ya kuwashirikisha watu wote katika utajiri, elimu na Iktisadi ilitia umaskini, ujinga na ubadhirifu wa Ardhi katika maumivu makubwa. Yamkini sasa umaskini, ujinga na ubadhirifu wa Ardhi unakaribia kufa. Tuliambiwa kuwa waganga katika ardhi walishughulika sana katika kutafuta njia ya kuyakomesha maradhi yote. Walikwisha faulu katika juu ya ndui na maradhi mengine. Walipata pia kuzigundua asili nyingi za magonjwa. Asili hizo zilikuwa zikijaribiwa kuharibiwa kwa kila njia njema iliyowezekana. Watu hawa walipasa kisifiwa na kuigwa."

"Amini aliyaona maeneo makubwa ya maji yaliyoitwa bahari, mapana yaliyoitwa maziwa, na marefu yaliyoitwa mito. Rangi na ladha za maji hayo zilikuwa mbalimbali. Kwa kuwa Kusadikika ilikuwa juu ya Ardhi, aliyashuku maji hayo kuwa ilikuwa damu ya wasadikika iliyokuwa ikimwagika kila siku. Alipowaona watu wa Ardhi wakinywa maji hayo, aliwafikiri kuwa walikuwa wakali na wabaya. Baadaye aliingiwa na haya moyoni mwake alipowaona kuwa walikuwa wapole na wema. Ukarimu ulikusudiwa kuenezwa huko kama jua lienezavyo nuru yake hapa. Hili ni tendo moja kubwa kabisa katika bidii za wanadamu. Amini hakufikiri kuwa hili litafaulu. Lakini alihakikishiwa kuwa kufaulu kwake kutatokana na kufahamiana kwa watu. Wakati mwingine watu wa Ardhi walikuwa wakali, lakini mara kwa mara waliweza kuitawala hasira yao. Amini aliposema kuwa alidhani walikuwa wakinywa damu ya wasadikika waliokuwa wakifa vitani, au kuchinjwa kwa kuua walistaajabu sana."

"Walijibu kuwa, kwa desturi, damu ilikuwa nyekundu na nzito kuliko maji. Walikuwa wakinywa maji meupe na mepesi na si damu. Amini alisema kuwa sababu ya kukosekana rangi katika kinywaji chao ilikuwa damu yenyewe ilikuwa ikivuja kutoka mbali sana. Ilichujuka rangi yake kwa upepo ikawa nyepesi kama maji. Maji ya Kusadikika yalikuwa meupe kama theluji, na yaliyo mepesi kama hewa. Watu wa Ardhi walinena kuwa maji yaliyo meupe kama theluji si maji ila theluji, na yaliyo mepesi kama hewa si maji ila hewa. Jibu likisadifu swali shaka huondoka. Amini hakuwa

na shaka tena juu ya kinywaji cha watu wa ardhi. Alisema moyoni mwake kuwa Ardhi iko chini ya Kusadikika lakini, akili ya watu wake ilikuwa juu ya ile ya wasadikika. Alicheka sana. Alijiona kama kwamba hakusema kweli au aliyeshindwa kuyathibitisha maneno yake. Watu wa Ardhi walipomuona anacheka, nao wakacheka vilevile."

"Kwa habari ya wasadikika waliokuwa wakifa vitani, Amini aliarifiwa kuwa zamani Ardhi ilikuwa ikitumia vita ili kuamua ugomvi kati ya pande mbili. Namna hii ya kuamua ilidumu muda wa karne nyingi bila ya kuhojiwa. Ilipoonekana kuwa mwenye haki kama hana nguvu alishindwa, na mwenye nguvu japo hana haki alishinda, maamuzi haya hayakuwafurahisha watu. Ushindi wa kulazimisha kwa nguvu ulikuwa kazi bure kwa mioyo iliyotaka haki. Vita namna mbalimbali vilitokea. Vita vidogo vilifuatwa na amani ndogo, na vikubwa amani kubwa. Amani hizo zilikuwa za kitambo tu. Kila amani ilikuwa ikiandaa vita vipya. Upande ulioshindwa ulikusanya nguvu juu ya upande ulioshinda. Mara kwa mara nguvu zilizokusanywa zilipotea bure kwa sababu vita vingine vililazimu kutokea tena. Kisasi kilisabiki nia za mataifa, uharibifu wa maisha ya watu ukaenea. Salama iliadimika kila mahali. Vita havikupungua katika Ardhi mpaka watu wake walipogundua kuwa hapana upande mmoja uliotamani kupigana na mwingine kama mapatano ya upole yaliwezekana kufanyizwa; wala mtu mmoja aliyependa kumwua adui kama iliwezekana kupatana naye. Amini aliposema kuwa hasira ya wasadikika ilikuwa haisikilizi hoja, aliambiwa kuwa hasira isiyosikiliza hoja huandamwa na kisasi kisichokwisha."

"Juu ya kuwachinja mahabusi kwa kuua, mjumbe wetu alisikia kuwa adhabu kama hiyo ilitumiwa sana zamani katika Ardhi. Wakati huo mashtaka yalikuwa hayachujwi. Mchujo wa mashtaka ulipohalalishwa katika sheria zao, mambo yalibadilika sana. Baadhi ya watu walituhumiwa kuwa walikuwa wahalifu walionekana, kwa kuchuja mashtaka yao, kuwa walikuwa si wahalifu kamwe. Walisingiziwa bure. Jambo hili lilipunguza sana machinjo ya washtakiwa. Adhabu ya kifo ilikusudiwa kubatilishwa katika sheria za Ardhi mara watu wake walikoma kuuana wenyewe. Bidii ya kuwafunza watu jinsi ya kutendeana wenyewe ilianza siku nyingi huko. Kila mtu alijitahidi kupingana na majaribu mabaya kwa nguvu zake zote. Hapana shaka Ardhi itakuwa mahali bora kwa maisha ya watu."

“Kwa rai zilizotolewa na watu wa Ardhi, na kwa mvuto wa ufanisi wao, mjumbe wetu alikuwa na haki ya kuitaka Kusadikika kuiga mwendo wa Ardhi. Katika maendeleo ya wanadamu Ardhi imekwenda hatua nyingi sana mbele kuliko ilivyofanya Kusadikika. Karibu maisha ya malaika yatafikiwa na watu wa Ardhi kama bidii zao zitafululiza. Hawana mabawa, lakini huruka hewani kama ndege kwa vyombo. Hawana mapezi, lakini huzama baharini kama samaki kwa vyombo vilevile. Umbali wa safari umekunjwa baharini, barani na hewani. Vitabu vyao vimeyakusanya mambo mabaya kwa ushahidi mwingi, na yaliyo mema kwa uangalifu mkubwa. Ushahidi wa mambo mabaya huwahadharisha juu ya misiba, na ule wa mambo mema huwahimiza kuenda mbele. Kwa njia hii, wamefaulu katika mambo mengi sana. Sasa shetani ana wivu juu ya watu wa Ardhi kwa sababu hawashawishiki tena upesi kama walivyokuwa zamani.

“Watu wenyewe walihitilafiana kwa rangi, lakini kwa akili zao za namna ya ajabu walipatana sana. Pia walihitilafiana na wasadikika kwa uzazi. Wanawake wetu huzaa mapacha lakini wao ni nadra sana kufanya hivyo. Maisha ya watoto wetu wengi hayana salama kuliko maisha ya watoto wao kidogo yalivyokuwa. Watu hao walisema lafudhi mbalimbali zilizoonyesha matokeo ya mchafuko wa lugha usemwao kuwa ulitokea zamani katika Ardhi lakini jitihada zote zilikuwa zikifanyika ili waweze kusikilizana kama watu wenye lugha moja tu. Yamkini hilo litawezekana kwa sababu watu wa huko wana bidii inayowaka kama moto. Wanaume kwa wanawake walizungumza habari za bidii, na kufanyiza bidii wakati wote. Kwa ubongo wao hutunga na kutangua mambo mpaka wapate jambo la kufaa. Kwa kano zao hujitwika na kujitua dhima kubwa na nzito. Walipata kusikiwa wakisema kuwa kwa sababu ya ujinga, kutofahamiana, wivu na chuki walipotelewa na hazina bora walizokuwa nazo zamani. Waliazimu kulitenda kila neno lililowezekana mpaka hazina iliyowapotea kwa wimbo wa shetani irudi tena katika mikono yao. Hazina hizo zilitakiwa kwa matumizi ya shirika ya watu wote. Kwa mambo kama haya, mjumbe wetu hakuweza kujizuia kuingiwa na fikira kuwa mwishoni watu wa Ardhi watakuwa na imani moja, taifa moja, hali moja na lugha moja kwa sababu hawakuamuru kosa lililowezekana kusahihishwa kumea kati yao.

Nusu moja ya safari yao ndefu imekwisha pitwa. Sasa wanakaribia kituo. Mashaka katika Ardhi karibu yatatoweka kama watu wake watashikilia

bidii kama gurudumu lao. Amini alirudi hapa kutoa habari hizi kwa sababu alikijua kima hasa cha heshima. Kama asingalijua heshima ni nini, asingalirudi tena kushiriki pamoja na sisi mashaka ya Kusadikika."

"Katika nchi nyingine mjumbe kama huyu asingalitoka katika makumbusho ya heshima. Angalichorwa kwa sanamu ya mawe. Sanamu hiyo ingalisimamishwa juu ya kila njia kuu kuwaashiria watu wengine kutenda kama alivyotenda yeye kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya nchi yao. Jina lake lingalikaririwa na kila kinywa cha kizazi kipya. Lakini yeye hakupata shukrani ya nchi hii kwa kazi yake bora. Alidhihakiwa kuwa ujumbe wake haukuleta faida, akahukumiwa na baraza kunyang'anywa milki yake na kifungo cha maisha. Kosa hili limetendwa hapa mara kwa mara. Kwa desturi, kosa hufanyika upesi sana kuliko liwezekanavyo kutengenezwa, na hujificha sana kuliko liwezekanavyo kugunduliwa; lakini likigunduliwa lazima kulisahihisha bila ya ajizi. Hii ndiyo sababu yangu ya kutaka uanasheria kupewa nafasi ya kuhalalishwa katika Kusadikika."

"Nimeshtakiwa kuwa nataka ufalme na kupingana na sheria. Sitaki jambo hata moja katika mambo haya mawili. Sharafa ya sheria ni kubwa sana. Nimo katika zizi lake kama ng'ombe. Sina budi kuitii. Ng'ombe aliyevunjika mguu malishoni, hujikokota zizini kusaidiwa. Kwa kuchechemea wajumbe wetu wamerudi zizini kutoka safari ndefu lakini hawakusaidiwa."

# HUKUMU

Mfalme wa Kusadikika aliwaambia madiwani. "Waungwana, sisi sote tumesikia ushahidi wa waziri, badala ya serikali ya Kusadikika, na ule wa Mudir wa sheria, mahali pa serikali ya Kusadikika vilevile. Ushahidi huu ulichukua muda wa siku moja. Kadhalika tumeyasikia maombezi ya mshtakiwa yaliyochukua karibu muda wa juma moja. Sasa tuna hiari mbili za kuchagua, yaani, kuiahirisha kesi hii mpaka ushahidi mwingine upatikane, au kuikata kwa ushahidi uliopatikana. Katika njia hizi mbili, mimi nataka sana njia ya pili. Sababu zangu za kufanyiza hivyo ni kuwa ushahidi tulio nao umetoka kwa mashahidi walio mahiri au stadi sana katika sheria za nchi hii. Wa kwanza amehitimu ubalozi, na wa pili ni mufti katika ukadhi. Wote wawili ni watu mashuhuri sana. Mashahidi hawa hawakuonyesha dalili yoyote kuwa ushahidi mwingine ulilazimu. Kwa hivi naona kama kwamba hawakuwa na neno jingine la kuongeza. Kama hili likiwaafiki kazi yetu itupasayo itatimizwa. Mwasemaje, waungwana?"

"Madiwani walikuwa wamechoka kukaa kitako kwa muda mrefu. Wote walitaka kesi imalizike ili waende kwenye kazi zao nyingine. Walipodhihirisha hili kwa umoja mfalme alitamka, "waungwana, sitawacheleweshsa kwa hotuba ndefu. Jambo nipasiwalo nalo sasa ni kujumlisha ushahidi kwa maneno machache sana na kuyaonyesha jinsi ulivyohusiana na mashtaka yaliyoletwa mbele ya baraza hii."

"Imesemwa kuwa mshatakiwa alidai uanasheria kuhalalishwa katika Kusadikika. Katika maombezi yake yote, yalikuwa na wingi wa maneno mema, jaribu la kuyakanusha madai haya halikufanyizwa. Kwa kuwa uanasheria haukujulikana hapa zamani, inakubalika kabisa kuwa mshtakiwa alitaka kuuleta, na hasa aliileta elimu ngeni. Kwa tafsiri ya mashahidi tuliambiwa kuwa elimu hii ilikuwa pingamizi katika sheria zilizohalalishwa. Kuipinga sheria kwenda katika njia yake ya haki ni uhalifu mkubwa kabisa. Hapana mtu hata mmoja anayeweza kufanyiza pingamizi katika sheria bila ya kustahili adhabu maalumu. Katika kesi hii mathibitisho ya uhalifu hayakupatikana. Baraza ilibatilisha tafsiri ya mashahidi kwamba ilikuwa si wazi sana kuliko ile ya mshtakiwa iliyosema

kuwa uanasheria ulikuwa ni elimu ya uamuzi kwa mujibu wa sheria. Mshtakiwa alisema kwa kujua. Alizitoa sababu zake, na sababu zenyewe zilikuwa njema kama ilivyoonekana katika maombezi yake yote. Kwa kweli, jambo lililo muhimu, ni lazima tufanyize uamuzi wetu wenyewe juu ya neno lithibitikalo, siyo lifikirikalo lakini halithibitiki. Dhana ya kuwa kila kitu kigeni ni pingamizi au kibaya inataka mathibitisho. Kama mathibitisho hayapatikani, fikira hiyo lazima ibatilike. Mathibitisho yaliyopatikana katika kesi hii hayausaidii ushahidi ila maombezi:

Kwa hivi nawaachia nyinyi, waungwana, mfikiri juu ya ushahidi huu na mtakavyoafikiana juu ya uamuzi."

Madiwani hawakukawia kuafikiana juu ya uamuzi. Baada ya kusemezana kwa muda wa dakika chache, mkubwa wao alisema kuwa wameafikiana kwa umoja juu ya uamuzi wao. Mfalme aliuliza. "Uamuzi gani mlioafikiana?" Walijibu

"Twaona kuwa mshtakiwa hana hatia, ila alikuwa akitafuta jinsi ya kuisaidia sheria ya Kusadikika kwa njia ngeni."

Mfalme alinena. "Taibu, hiyo ni hukumu njema. Naafikiana na nyinyi kabisa hapana hukumu nyingine iliyowezekana juu ya ushahidi uliokuwa mbele yetu. Zaidi ya hayo, natoa amri kuwa watu sita waliotajwa katika kesi hii-Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini-wafunguliwe mara moja. Inasikitisha sana dhuluma juu ya watu hawa hazikutengenezwa mpaka leo. Gereza ni makao ya wahalifu. Watu hawa si wahalifu ila wafadhili bora. Wanastahili uhuru na heshima kubwa. Hasara zao lazima zifidiwe. Kusadikika inamshukuru sana Karama kwa kuitanabahisha wajibu wake."

Mwisho wa maneno ya mfalme ulivunja baraza. Watu walisimama wakaenda zao. Baada ya miaka michache kupita, mazungumzo yote yaliyoletwa Kusadikika na wajumbe wake yaliziamsha bidii zilizokuwa zimelala. Mavuno ya mafunzo hayo yaliifanya Kusadikika kuwa nchi moja katika nchi zilizositawi kabisa.

Ni hayo yaliyotokea huko kwa nchi ya wasadikika.

# TAMATI